**RAIS SAMIA ASHIRIKI MKUTANO WA KAMATI YA WAKUU WA NCHI NA SERIKALI KUHUSU MABADILIKO YA TABIANCHI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshiriki Mkutano wa Kamati ya Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika inayosimamia Mabadiliko ya Tabianchi (The Committee of the African Heads of State and Government on Climate Change-CAHOSGCC) uliofanyika pembezoni mwa Mkutano wa 38 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika jijini Addis Ababa, Ethiopia, tarehe 16 Februari 2025. Mkutano huo umefanyika kufuatia mwaliko wa Mwenyekiti wa Kamati hiyo ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Kenya, Mhe. Dkt. William Ruto umejadili jitihada mbalimbali za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na mikakati ya kuhakikisha nchi za Afrika zinapata fedha kwa ajili ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Mhe. Ruto ameipongeza Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanikisha Mkutano wa Wakuu wa Wakuu wa Nchi na Serikali kuhusu Nishati Barani Afrika (Mission 300) uliofanyika mwezi Januari, 2025 na kueleza kuwa mkutano huo ulijadili fursa, changamoto na kupitisha maazimio yatakayowezesha upatikanaji wa nishati ya uhakika na kwa gharama nafuu. Kadhalika, ameeleza Mkutano wa Mabadiliko ya Tabianchi Afrika uliofanyika mwezi Septemba 2023 Nairobi, Kenya ulijadili njia mbalimbali za kupunguza utoaji wa gesi chafu na mbinu za kukabiliana na athari za hali ya hewa, sambamba na uwekezaji katika nishati jadidifu na kuongeza ushirikishwaji wa wabia wa kimataifa ili kuongeza fedha za miradi ya nishani barani Afrika. Mkutano huo pia umepitisha maazimio ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali kuhusu Nishati ( Heads of State Energy Summit) na kuyawasilisha katika mkutano wa 38 wa Wakuu wa Nchi na Serikali.